NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Riḍván 2018

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Tunawasalimu katika mng'ao unaoendelea kudumu wa yale matukio ya kukumbukwa ambayo yalienzi miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Uzuri Uliobarikiwa. Wakati tunapofikiria yale yaliyotukia wakati huo na tangu hapo, tunaona kwamba jumuiya ya Kibahá'i ya ulimwengu inavyoonekana sasa si sawa na ilivyokuwa wakati ilipoanza duru sita za mwanzo za Mpango wa sasa. Inatambua zaidi kuliko wakati wowote hapo kabla juu ya dhima yake. Imepitia mtapakao ambao haujawahi kutokea katika uwezo wake kuwaleta marafiki na jamaa karibu na maisha yake ya kijumuiya; kuvuvia ujirani na vijiji katika jitihada ya pamoja; kuelezea kwa ufasaha jinsi kweli za kiroho zinavyoweza kutafsiriwa katika vitendo endelevu; na, juu ya yote, kuzungumza si tu kuhusu mafundisho ambayo yataujenga upya ulimwengu, lakini kumhusu Yeye Ambaye alifundisha hayo: Bahá'u'lláh. Maelezo ya maisha Yake na ya mateso Yake yaliyosimuliwa kwa lugha nyingi na watu wazima, vijana, na watoto yaligusa mioyo isiyo na idadi. Baadhi walionesha wenyewe wapo tayari kuchunguza zaidi Hoja Yake. Wengine waliahidi ushirikiano. Na roho nyingi pokevu zilisukumwa kukiri imani.

Kiashirio elekezi kimojawapo cha maendeleo kilikuwa ni sehemu nyingi ambako ilikuwa dhahiri kwamba Imani iliibuka kutoka kutotambulika kwenye ngazi ya kitaifa. Kulikuwa na viongozi wa serikali na viongozi wa fikra ambao walitamka—na wakati mwingine walisisitiza faraghani—kwamba ulimwengu upo katika uhitaji wa muono wa Bahá'u'lláh na kwamba jitihada za Wabahá'í zinapendwa na hazina budi kupanuliwa. Ilitufurahisha kuona kwamba hawakuwa Wabahá'i pekee ambao walipenda kumuenzi Bahá'u'lláh na kusherehekea maisha Yake—mikusanyiko maalum iliandaliwa na baadhi kutoka nje ya jumuiya ya Kibahá'í. Katika maeneo ambako kuna uhasama kwa Imani, marafiki hawakufadhaishwa; wakionesha uthabiti wa kustaajabisha, waliwatia moyo raia wenzao kuchunguza ukweli wao wenyewe, na wengi walishiriki kwa shangwe katika maadhimisho. Sherehe hii ya miaka mia mbili pia ilisababisha mwonekano wa uchanuaji usio na kikomo wa maonesho ya kisanii, ushuhuda adhimu kwa chemchemi ya upendo ambamo ilitokea. Sifa bainifu ya namna ambayo jumuiya ya Kibahá'í ililiendea tukio hili ilikuwa ni uthibitisho wa mafunzo yaliyopatikana kwa zaidi ya miongo miwili sasa, tangu mfululizo wa sasa wa Mipango ya ulimwengu ulipoanza. Mtu binafsi alichukua hatua, jumuiya iliinuka katika jitihada ya pamoja, na marafiki walielekeza nguvu zao za kiubunifu kwenye mipango iliyoandaliwa na asasi. Kumbukumbu muhimu, ikiashiria kupita kwa karne mbili, ilitoa kichocheo chenye nguvu kwa kazi ya ujenzi wa jumuiya kwa karne ijayo. Katika kipindi kuelekea kwenye sherehe ya pili ya miaka mia mbili, hebu kila mbegu iliyopandwa kwa upendo mkuu kwenye ile ya kwanza ilelewe kwa uvumilivu kuelekea utoaji matunda.

Miaka miwili ndani ya Mpango wa sasa, ingawa kwa kawaida maendeleo hayafanani kutoka nchi hadi nchi, idadi ya programu zenye ukuaji wa nguvu ulimwenguni inakaribia nusu ya zile elfu tano zilizokusudiwa katika juhudi ya sasa ya ulimwengu, na kiwango ambacho idadi hii inaongezeka kimekuwa kikiongezeka daima. Kuangalia kwa ukaribu zaidi, kuna dalili za matumaini za jinsi nguvu na uwezo wa watu binafsi, jumuiya, na asasi zinavyodhihirika. Kwa waumini kila mahali, tajiriba ya sherehe ya miaka mia mbili ilionesha kwamba maingiliano yao mengi ya kila siku na watu wanaowazunguka yanaweza kuchanganywa na moyo wa ufundishaji. Na kadiri kazi katika maelfu ya vijiji na ujirani inavyojikusanyia nguvu mwendo, maisha ya kijumuiya yenye msisimko yanajikita mizizi katika kila moja. Idadi ya klasta ambako mfumo kwa ajili ya upanuzi wa ruwaza hii ya shughuli hadi kwenye maeneo zaidi na zaidi inaimarika vyema—hapo, ikiwawezesha marafiki kuvuka hatua ya tatu ya ukuaji sanjari na mwendelezo wa maendeleo—imekua kwa udhahiri. Na ni hapa, kwenye wigo wa ujifunzaji wa ulimwengu wa Kibahá'í, hususani katika mjongeo wa watu kuelekea muono wa Bahá'u'lláh, ambapo si tu idadi kubwa inakuja kwenye ukumbatiaji mpana wa shughuli za Kibahá'í bali marafiki sasa wanajifunza jinsi makundi makubwa yanavyokuja kujitambulisha yenyewe najumuiya ya Jina Kuu Kabisa. Tunaona jitihada za kielimu za Imani zikichukua sifa bainifu rasmi zaidi katika maeneo kama hayo, kadiri watoto wanavyoendelea kupitia madaraja mwaka hadi mwaka bila kikwazo na kiwango kimoja cha programu ya uwezeshaji kiroho wa vijana chipukizi kinavyokifuatia kingine bila kukosa. Katika maeneo haya, taasisi ya mafunzo inajifunza kuhakikisha kwamba rasilimali watu ya kutosha inakuzwa ili kutoa uadilishaji wa kiroho na kimaadili wa watoto na vijana chipukizi kwa idadi iongezekayo daima. Ushiriki katika shughuli hizi za kimsingi unakuwa uliotiwa ndani sana katika utamaduni wa watu kiasi kwamba unaonekana kama vile kipengele cha lazima cha maisha ya jumuiya. Uhai mpya huibuka ndani mwa watu wanaochukua jukumu la maendeleo yao wenyewe, na wanajenga kinga kwa zile nguvu za kijamii ambazo huzaa ubaridi. Uwezekano kwa ajili ya maendeleo ya kimwili na kiroho hupata umbo. Uhalisia wa kijamii huanza kubadilika.

Marafiki mpendwao mno, huu kwa kweli ni wakati wa kutoa shukrani kwa Mpendwa-Kabisa. Kuna sababu kubwa nyingi za kutiwa moyo. Walakini tunafahamu vyema tu juu ya ukubwa wa kazi ambayo imebakia. Kimsingi, kama tulivyoonesha hapo awali, lazima liibuke katika mamia ya klasta kundi likualo la marafiki ambao wanaweza kudumisha, pamoja na wale wanaowazunguka, umakinikiaji endelevu juu ya uleaji wa ukuaji na kujenga uwezo, na ambao wamepambanuliwa kwa uwezo wao na nidhamu yao kutafakari juu ya utendaji na kujifunza kutokana na tajiriba. Uinuaji na uambatanaji na kiini kipanukacho cha watu binafsi katika kila mahali—si tu kwenye ngazi ya klasta bali ndani ya ujirani na vijiji—papo hapo ni changamoto ya kuogofya na hitaji muhimu sana. Lakini pale ambapo hili linatokea, matokeo hujieleza yenyewe.

Tunatiwa moyo kuona kwamba asasi za Imani zinaweka hitaji hili la juu kabisa mstari wa mbele wa ufikiri wao, zikibuni taratibu zifaazo kuwezesha umaizi unaopatikana kutokana na maendeleo utumike kwa mapana. Wakati huo huo, tajiriba kubwa zaidi inayapatia mashirika ya kitaifa, kikanda, na mahali kadhalika muono mpana zaidi. Yanaanza kujishughulisha katika nyanja zote

za maendeleo ya jumuiya na yanahusika na ustawi wa watu nje ya washiriki wake rasmi. Yakiwa na utambuzi wa matokeo ya kina ambayo mchakato wa taasisi unayo kwa ajili ya uendelezaji wa watu, yanaweka umakini maalumu kwenye namna taasisi ya mafunzo inavyoweza kuimarishwa. Yanabakia zingatifu kwa haja ya kudumisha umakinifu wa jumuiya juu ya mahitaji ya Mpango na kulialika kundi lipanukalo daima la marafiki kwenye viwango vya juu zaidi na zaidi vya umoja. Kwa uaminifu yanashikilia jukumu lao la kuboresha mifumo yao ya kiutawala na kifedha ili kwamba kazi ya upanuzi na uimarishaji iweze kusaidiwa vyema. Katika yote haya, hatimaye yanajishughulisha na kutengeneza katika jumuiya yale mazingira ambayo hufaa kwa ajili ya uachiliaji wa nguvu za kiroho zenye uwezo.

Kadiri kazi ya ujenzi wa jumuiya iongezekavyo nguvu, marafiki wanatumia ule uwezo mpya walioukuza kuboresha hali katika jamii inayowazunguka, shauku yao ikiwashwa kwa ujifunzaji wao wa mafundisho matakatifu. Miradi ya muda mfupi imeongezeka mno kwa idadi, programu rasmi zimepanua wigo wao, na sasa kuna mashirika zaidi ya maendeleo yenye muelekeo wa Kibahá'í yanayojishughulisha na elimu, afya, kilimo, na maeneo mengine. Kutokana na matokeo ya mabadiliko yaonekanayo katika maisha ya mtu binafsi na ya pamoja ya watu kunaweza kuonekana msisimko bayana wa nguvu ya ujenzi wa jamii ya Hoja ya Bahá'u'lláh. Hapana shaka, hivyo, kwamba ni kutokana na mifano kama hiyo ya vitendo vya kijamii —viwe rahisi au tata, vya muda maalumu au vya muda mrefu—kwamba Ofisi za Jumuiya ya Kimataifa ya Kibahá'í zinaongeza kuchukua uvuvio katika jitihada zao kushiriki katika mijadala iliyopo ya kijamii. Huu ni uga mwingine muhimu wa jitihada kwa Imani ambao umepiga hatua vyema. Kwenye ngazi ya kitaifa, michango kwenye mijadala ambayo ina maana kwa jamii hiyo—usawa wa wanaume na wanawake, uhamiaji na uunganishaji, wajibu wa vijana katika mabadiliko ya kijamii, na kuishi pamoja kidini chanjari, miongoni mwa mengine—inafanyika kwa ujasiri ukuao, ustadi, na umaizi. Na popote wanapoishi, kufanyakazi, au kusoma, waumini wa rika zote na usuli wanatoa michango yenye thamani kwa mijadala maalumu, wakileta kwenye utambuzi wa wale wawazungukao mtazamo wa kikanuni uliobumbwa na Ufunuo mpana wa Bahá'u'lláh.

Msimamo wa Imani katika nafasi mbalimbali ambamo mijadala inafunguka kwa kiasi kikubwa umezidishiwa nguvu kwa uwepo wake rasmi kwenye Tovuti ya Ulimwengu Mzima, uwepo ambao umepanuka kwa kiasi kikubwa kupitia uzinduzi wa tovuti nyingi za Kibahá'í za kitaifa na uendelezaji zaidi wa familia ya tovuti zihusianazo na Bahai.org. Hii ina thamani kubwa sana kwa vyote uenezaji na ulinzi wa Hoja. Katika kipindi cha siku chache tu hadhira kubwa ya dunia ilivutiwa na maudhui yaliyoandaliwa kwa umakini kuhusu Imani ambayo yaliwasilishwa kwenye tovuti ya tukio la miaka mia mbili na kuandikwa katika lugha tisa sanjari, na ambayo sasa imeongezewa kurasa za nchi moja moja zikielezea kwa kifupi anuwai za maadhimisho ambayo yalitokea. Mipango tayari imekwishaandaliwa kwa ajili ya kutambulisha kwenye tovuti ya Maktaba ya Kibahá'í ya Marejeo muundo ambao utaruhusu kurasa ambazo hazikutafsiriwa na kuchapishwa hapo awali au Nyaraka kutoka Maandiko Matakatifu kuachiliwa mtandaoni kadiri muda unavyoenda. Sambamba na hili, vitabu vipya vya Maandiko ya Bahá'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá vilivyotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza vimepangwa kuonekana katika miaka ijayo.

Huko Santiago, Chile, na Battambang, Cambodia, Nyumba za Ibada za ulimwengu zilizozinduliwa hivi karibuni zaidi_zinakuwa vituo madhubuti vya mvuto, minara kwa jamii zao ya yale yote ambayo Imani_hushikilia. Na idadi yao inakaribia kukua. Tunayo furaha kutangaza kwamba sherehe ya uzinduzi wa Hekalu la Norte del Cauca, Colombia, itafanyika Julai. Zaidi, ujenzi wa Nyumba za Ibada zaidi upo karibuni tu. Huko Vanuatu, kibali kipo mbioni kupatikana ili kuanza kujenga. Huko India na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mchakato tata kabisa na wenye changamoto hatimaye umesababisha mafanikio ya upatikanaji wa ardhi. Shangwe baada ya kuona mchoro wa Mashriqu'l-Adhkár ya kwanza ya kitaifa ikifunguka huko Papua New Guinea wakati wa Naw-Rúz ilikuwa haijazimika pindi mchoro wa Nyumba ya Ibada ya mahali ya Kenya ilipofunuliwa pia. Wakati huo huo, tuna kila matarajio kwamba tamko na makusanyo vilivyotolewa hivi karibuni kuhusu asasi ya Mashriqu'l-Adhkár vilivyoandaliwa na Idara yetu ya Utafiti, vitachochea zaidi utambuzi wa marafiki wa umuhimu wa ibada katika maisha ya jumuiya. Kwani kwa vitendo vyao vya huduma, hususani katika mikusanyiko yao ya ibada ya mara kwa mara, Wabahá'í kila mahali wanaweka misingi ya kiroho ya Nyumba za Ibada za baadaye.

Ni miaka mitatu tu imebakia ya jitihada ya robo karne iliyoanza mwaka 1996 iliyojikita kwenye lengo moja: uendelezaji wa kutambulika katika mchakato wa uingiaji kwa makundi. Mnamo Riḍván 2021, wafuasi wa Bahá'u'lláh wataanza Mpango utakaodumu kwa mwaka mmoja. Mfupi, lakini wenye wingi wa maonyo, jitihada hii ya mwaka mmoja itaanzisha wimbi jipya la Mipango ikiibeba safina ya Hoja kuingia karne ya tatu ya zama za Kibahá'í. Wakati wa kipindi cha miezi hii kumi na mbili yenye heri, maadhimisho ya Kibahá'í ya ulimwengu_ya miaka mia moja ya Kupaa kwa 'Abdu'l-Bahá yatajumuisha mkusanyiko maalumu kwenye Makao Makuu ya Ulimwengu ya Kibahá'í ambako wawakilishi wa kila Baraza la Kiroho la Kitaifa na kila Halmashauri ya Kibahá'í ya Kanda wataalikwa. Huu, walakini, utakuwa ni wa kwanza tu katika mfululizo wa matukio ambayo yatawaandaa waumini kwa matakwa ya miongo itakayokuja. Januari itakayofuata, kumalizika kwa miaka mia moja tangu usomaji wa mara ya kwanza wa Wasia na Agano la Bwana kwa umma kutakuwa ni tukio kwa ajili ya kongamano katika Nchi Takatifu likizileta pamoja Bodi za Washauri wa Bara na wajumbe wote wa Bodi Saidizi kwa ajili ya Ulinzi na Uenezaji. Nguvu ya kiroho itakayoachiliwa kwenye mikusanyiko hii miwili ya kihistoria kisha lazima ipelekwe kwa marafiki wote wa Mungu katika kila nchi wanamoishi. Kwa kusudi hili, mfululizo wa makongamano utaitishwa kote ulimwenguni katika miezi itakayofuatia, kichocheo kwa jitihada ya miaka mingi ambayo itafuatia Mpango wa Mwaka Mmoja ujao.

Hivyo, awamu mpya katika ukunjukaji wa Mpango Mtakatifu wa Bwana inakaribia. Lakini matarajio ya kusisimua na_ya haraka zaidi yapo moja kwa moja mbele. Miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Báb ni mwaka mmoja na nusu tu kutoka sasa. Hiki ni kipindi cha kukumbuka ushujaa usio wa kawaida wa Mfia-Dini Mtangulizi wa Imani yetu, Ambaye utume Wake wenye matukio uliwasukuma wanadamu kuelekea zama mpya za historia. Ingawa imetofautishwa kutoka wakati wetu kwa karne mbili, jamii ambamo Báb alitokea hufanana na ulimwengu wa siku hizi kwa namna ya ukandamizaji na kwa shauku ya wengi kutafuta majibu ili kuzima kiu ya roho

kutaka kujua. Katika kufikiria jinsi gani kumbukumbu ya miaka hii mia mbili inavyoweza kuadhimishwa ifaavyo, tunatambua kwamba maadhimisho haya yatakuwa na sifa bainifu maalumu ya namna yake. Hata hivyo, tunatarajia kushamiri kwa shughuli zisizo pungufu ya ubora na uhusishaji kuliko zile ambazo ziliambatana na tukio la miaka mia mbili lililopita hivi karibuni. Ni tukio ambalo kila jumuiya, kila kaya, kila moyo bila shaka watatazamia kwa matarajio yenye ari kubwa.

Miezi ya mbele pia utakuwa ni wakati kwa ajili ya kujikumbusha maisha ya wafuasi jasiri wa Báb—mashujaa wa kike na wa kiume ambao imani yao ilioneshwa katika vitendo visivyo kifani, vya kujitoa dhabihu ambavyo daima vitazipamba kumbukumbu za kihistoria za Hoja. Sifa zao za utovu wa woga, kujiweka wakfu, na kujitenga kutoka vyote isipokuwa Mungu humgusa kila mmoja ambaye hujifunza kuhusu vitendo vyao vya uthubutu. Kinachoshangaza, vile vile, ni umri mdogo ambamo kwao wengi mno wa hao wenye ujarisi walipoweka alama yao isiyofutika katika historia. Katika kipindi kinachokuja, hebu mfano wao uweze kuleta ujasiri kwa kundi zima la waaminifu—hususani kwa vijana, ambao kwa mara nyingine tena wanaitwa kwenye kikosi cha mbele cha mjongeo ulichokusudiwa si kwa kingine isipokuwa mabadiliko ya ulimwengu.

Hili, hivyo, ni tumaini letu angavu, angavu. Katika duru sita zilizopo kati ya Riḍván hii na tukio lijalo la miaka mia mbili—kwa hakika, kwa miaka yote mitatu iliyobakia ya Mpango wa sasa—hebu upendo ule ule uteketezao vyote, upitao vyote ambao uliwachochea wanafunzi wa Báb kwenye uenezaji wa mwanga mtakatifu uwavuvie kwenye matendo makuu. Kwamba muweze kuwa wapokeaji wa msaada wa mbinguni ni maombi yetu kwenye Kizingiti Kitakatifu.

[Umesainiwa: Nyumba ya Haki ya Ulimwengu]